

## BUKU LA 18

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Ninatumaini kila mtu alikuwa na likizo ya kufana. Ijapokuwa mwaka huu unaweza kuonekana tofauti kwa familia zetu nyingi, ninahisi nina imani tunaweza kupata kitu cha kushukuru wakati wa msimu huu. Nina shukrani sana kwa Wanabodi wangu wa ajabu, wanafunzi, wafanyakazi, wasimamizi, waalimu, na wafanyakazi walio katika mstari wa mbele waliojitolea kusaidia jamii yetu kuendelea wakati huu.

Tafadhali hakikisha umeshiriki katika Mkutano wa Bodi Jumatatu hii, Desemba 7 ili usikilize maelezo ya ana kwa ana ya kurudi shule kwa viongozi, waalimu wakuu, waalimu, na wanafunzi wa wilaya. Maelezo haya yatasaidia washikadau wa jamii yetu kujiandaa kwa 2021 katika majira ya baridi na wawe Tayari kwa Shule za DeKalb kufunguliwa tena. Unaweza kutazama Mkutano wa Bodi kwenye kituo 24 katika Kaunti ya DeKalb au mtandaoni kwenye [DeKalb Schools TV](#). Pia tuna chaguo la video kwa wale ambao wangetaka kutazama baadaye.

Hivi karibuni nitakuwa nikishiriki Mpango wangu wa Siku 100 ikiwemo uwezo, nafasi na ahadi za DCSD. Ninafuraha kuhusu kushiriki matokeo yangu na kuendelea kukuza maono ya DCSD ya kutia moyo jamii yetu ya wanafunzi kufikia ufanisi wao wa kielimu.

### Taarifa ya COVID-19

Viwango vya maenezi katika jamii vinaendelea kuongezeka zaidi ya kigezo cha “Maenezi ya Juu” ya visa 100 kwa wakazi 100,000 kwa kipindi cha wiki mbili kama ilivyohesabiwa na Idara ya Afya ya Umma ya Georgia (GDPH). Hadi leo, nambari hii iliyoripotiwa na GDPH ya Kaunti ya DeKalb ni 323. Ili kupata habari mpya kuhusu viwango vya maenezi katika Kaunti ya DeKalb, tafadhali endelea kutembelea: <https://dph.georgia.gov/covid-19-daily-status-report>. Ijapokuwa tuna wasiwasi kuhusu kuongezeka kwa idadi hii, tutaendelea kuandaa masomo ya ana kwa ana na kukuza hatua wazi za usalama ili kuhakikisha wanafunzi na wafanyakazi wetu wamejiandaa kufungua shule kwa usalama.

Huku visa vikiendelea kuongezeka kwa kasi nchini Marekani, njia salama zaidi ya kusheherekea sikukuu ni kusheherekea nyumbani na watu wanaoishi nao kila siku. Kukusanyika na familia na marafiki ambao hawaishi na wewe kunaweza kuongezea uwezo wa kupata au kueneza COVID-19 au flu.

[Bofya hapa kwa baadhi ya vidokezo kutoka kwa CDC kuhusu jinsi ya kuwa salama wakati wa msimu huu wa likizo.](#)

### **Kuwezesha Familia na Kushirikisha Jamii**

Katika kutambua na kusheherekea mwezi wa Siku ya Kitaifa ya Kushirikisha Familia ya Nov 21, tulikuwa na [Kongamano la Mtandaoni la Kuwezesha Wazazi na Familia.](#) Mkutano huu uliwapa familia Vikao vya Habari vya Mtandaoni na hata pia rasilimali na wachuuzi wa dijitali. Asante kwa kila mtu aliyehudhuria kongamano na asante kwa Baraza la Ushauri wa Wazazi (PAC) kwa kukutana wiki hii. Ushirikiano huu unaendelea kuipa nguvu kijiji chetu. Tafadhali kuwa tayari kwa Mikutano zaidi ya Ukumbi wa Mji ya Waalimu Wakuu, Wafanyakazi na Familia kwa mwezi huu wa Desemba. Ikiwa unahitaji maagizo ya jinsi ya kufikia tukio la Microsoft Live, tafadhali tembelea hapa <https://www.dekalbschoolsga.org/featured-news/regional-parents-town-hall/>.

Nilikuwa na wakati mzuri katika hafla ya Latino American Association Latin Fever jana na ninamshukuru Afisa Mtendaji Mkuu (CEO) ambaye ni mwanachama wa kamati yetu ya ushauri. Shirika la Wamerika Walatino linafanya kazi nzuri katika jamii na tunashukuru.

Kama jamii na kijiji, sote tuko pamoja katika haya yote. Tafadhali tunza ustawi na afya yako na utiwe moyo kwamba DCSD itaendelea kukua na kuwa na nguvu hata zaidi.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris